

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE MHE. EDWIN M.  
MWANZINGA KATIKA MKUTANO WA ROBO YA NNE BARAZA KUU LA MADIWANI  
TAREHE 31/07/2018 KWENYE UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE.**

**Mhe. Mkuu wa Wilaya,  
Mhe. Makamu Mwenyeikitii,  
Wahe. Wabunge  
Wahe. Madiwani,  
Ndg. Viongozi mbalimbali,  
Ndg. Mkurugenzi,  
Ndg. Watendaji wa Halmashauri,  
Ndg. Mabibi na Mabwana (Wageni Waalikwa).**

Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujali sote kuwepo hapa leo hii katika mkutano huu wa kawaida wa baraza kuu la Madiwani kwa ajili ya kujadili taarifa za kamati zetu za kudumu kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2017/2018,tukiwa wazima wa afya.

Pia napenda kuwashukuru nyote mlionhudhuria katika baraza hili kwani inaonesha kuwa nanyi mnaguswa na shughuli zinazofanya na Halmashauri yetu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Wahe. Madiwani,**

Halmashauri yetu ni mionganini mwa Halmashauri ambazo zimeendelea kufanya vizuri katika swala zima la ukusanyaji mapato ambapo mpaka kufikia robo ya nne tumeweza kukusanya kwa asilimia 106.2 napenda nitoe pongezi zangu kwenu ninyi Waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi na watendaji kwa jitihada mlizoonyesha katika zoezi zima la ukusanyaji mapato kwani asilimia kubwa ya shughuli za Halmashauri zinaendeshwa kuititia makusanyo yetu wenywewe.

**Wahe. Madiwani,**

Adhma ya Halmashauri yetu ni kuhakikisha kuwa tunathibiti upotevu wa mapato lakini pia kuangalia mapungufu yaliyojitekeza katika vipindi viliviyopita na kuona ni kwa namna gani tunaboresha siku hadi siku ili tuweze kukusanya zaidi.

Aidha, adhma hii haitofikiwa ikiwa hatutahimiza swala la ushirikiano baina yetu. Niwaombe sana tushirikiane katika kuboresha lakini pia katika kuhakikisha kuwa hakuna upotevu wa mapato.

**Wahe. Madiwani,**

Sekta ya elimu nayo haipo nyuma kwani katika robo hii Halmashauri yetu iliwatahini wanafunzi 702, wanafunzi 694 waliweza kufaulu kwa daraja la kwanza mpaka la nne na wanafunzi 8 pekee ndio waliofeli amba ni asilimia 1% tuu. Ufaulu wa asilimia 99% ni ufaulu mzuri na wajuu kabisa hivyo nawapongeza sana lakini niwatake watendaji kutobweteka kwa ufaulu huu tukaze buti zaidi kwani mitihani ipo kila mwaka na lolote linaweza kutokea kati ya kupanda juu zaidi au kushuka.

**Wahe. Madiwani,**

Katika kipindi cha nyuma tumeona ni kwa jinsi gani Mji wa Njombe umeingiliwa na wimbi la wafanyabiashara pembezoni mwa barabara lakini pia maeneo ambayo siyo rasmi. Wafanyabiashara hawa wamekuwa wakiuchafua Mji wetu wenye sifa nzuri ya usafi.

Tumeona pia jitihada za Halmashauri za kuwaondoa katika maeneo hayo licha ya kuwepo changamoto za kugongana kwa mawazo. Kwa sasa tumedhamiria kuwaondoa na uzuri ni kwamba zoezi hilo limeshaanza na tunaona mabadiliko.

Niwaombe sana kila mtu katika nafasi yake ahakikishe kuwa wafanyabiashara hawa hawarudi tena barabarani na sehemu zisizo rasmi.

Mhe, Rais amekuwa akisisitiza wafanyabiashara kutafutiwa maeneo ya biashara, kwa upande wa Halmashauri yetu tunayo maeneo ya kufanya biashara yenyi miundombinu bora hivyo hatunabudi kuhakikisha kuwa wanaenda katika maeneo yaliyotengwa na kuacha Mji wetu uendelee kuwa katika mazingira salama kwani hii sio manufaa ya Halmashauri tuu lakini hata kwao kwani watakuwa huru kufanya biashara zao pasipo na usumbufo.

**Wahe. Madiwani,**

Katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU tumeshuhudia kampeni ya FURAHA YANGU ILIYOZINDULIWA NA MHE. MKUU WA MKOA WA NJOMBE CHRISTOPHER OLE SENDEKA KATIKA MKOA WETU, Kampeni hiyo inayolenga Kuhamasisha kupima VVU na kutumia ARV mapema imeanza hivyo niwatake kuchukua jukumu la kuwahamasisha wananchi katika maeneo yetu kuchukua hatua kwa kupima na pindi watakapogundulika na maambukizi waanze kutumia ARV mapema hiyo ndio maana ya kampeni hiyo ya furaha yangu.Tuhakikishe furaha hizi haziishi maeneo ya mijini tuzielekeze pia katika maeneo ya vijiji ambapo wengi wetu wahe.madiwani tunawakilisha maeneo hayo.

Aidha niwatake kuendelea kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa wa UKIMWI na kubaki njia kuu. Tukumbuke kuwa hali ya maambukizi katika Mkoa wetu bado si shwari.

**Mwisho Waheshimiwa Madiwani,**

Nichukue nafasi hii kuwashukuru Viongozi wote wa Ngazi za juu yaani Taifa, Mkoa, Wilaya, Vyama vyta Siasa, Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wote na Wananchi kwa namna ya pekee jinsi mnavyotoa ushirikiano katika maendeleo ya Halmashauri yetu. Ushirikiano na kujituma katika utendaji kazi iwe ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Halmashauri yetu.

**NAWASHUKURU SANA KWA KUNISIKILIZA  
NA BAADA YA KUSEMA HAYA, NATAMKA KUWA MKUTANO WA MWAKA WA ROBO YA  
NNE WA BARAZA KUU LA MADIWANI NIMEUFUNGUA RASMI.**

*Mhe. Edwin Mwanzinga*  
**MWENYEKITI**  
**HALMASHAURI YA MJII**  
**NJOMBE**